**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. MASWALI:

### Wizara ya Fedha na Mipango:

58. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Bodi ya Mapato ya Tanzania (TRA) wana mpango wa kuhamasisha ubandikaji wa stempu kwa wafanyabiashara katika bidhaa zao.

Je, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) imejipanga vipi kubandika stempu kama hizo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

124. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMED (Jimbo la Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Awamu ya Nane katika kipindi hiki cha pili (2025 – 2030) imedhamiria kuendelea kuimarisha miundombinu ya elimu kupitia ujenzi wa skuli, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya maabara, sayansi na teknolojia.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza zaidi katika

upatikanaji wa vifaa vinavyosaidia mafunzo ya Akili Mnemba (*Artificial Intelligence)* na *Computer Coding* kwa Skuli za Maandalizi na Sekondari, ili kuwawezesha wanafunzi kuendana na kasi ya mabadiliko ya dunia.

(b) Je, mitaala tunayoendelea nayo inaendana vipi na kizazi kilichopo na mwelekeo wa dunia au tunahitaji kuifanyia tathmni mpya.

186. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa vyuo vya Zanzibar wamekuwa wakipambana kuhusu kutumika kwa pasi ya somo la dini (Islamic) kuwa moja ya pasi inayotumika kwa mwanafunzi kujiunga katika vyuo vya kati bila ya manufaa.

(a) Ni lini Serikali itafanya tathmini kutambua idadi halisi ya vijana wa kizanzibari walioshindwa kujiunga na elimu ya Vyuo vya Kati, kwa kuwa na pasi nne (4) za Kidato cha Nne, ikiwemo pasi ya dini.

(b) Je, ni ipi sababu iliyopelekea kuondolewa kwa pasi ya dini kuwa moja ya kigezo cha mwanafunzi kujiunga na elimu ya juu.

<u>**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**</u>

35. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Serikali chini ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume ilianzisha *Television* Zanzibar (TVZ) ambayo ilikuja kufanyiwa mabadiliko na sasa kutambulika kama Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC). Shirika la Umma linaloendeshwa kwa kodi za wananchi wote wa Zanzibar bila ya kujali itikadi za vyama, makabila ama sehemu wanazotoka na kutoa habari za kuujulisha umma mambo mbali mbali yanayoendelea ulimwenguni.

(a) Ni kwa kiasi gani ZBC inatoa huduma zake bila ya upendeleo wa kisiasa pamoja na urushaji wa vipindi ama ‘air time’.

(b) Ni lini watendaji wa Shirika hilo watapewa mafunzo yatakayowawezesha kufanya kazi zao kwa weledi bila ya tashwishi za siasa.

(c) Ni upi mkakati wa Serikali wa kuimarisha zaidi Shirika hilo kongwe barani Afrika, ili kuweza kuingia katika soko la ushindani wa kurusha maudhui yake.

## Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:

56. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kuna utaratibu wa kila mwaka kwa watumiaji wa vyombo vya moto kukata leseni na vibali vya njia ili kuwaruhusu wao kutembea barabarani.

Je, kuna tofauti gani kati ya gari kubwa, gari ndogo na za kawaida wakati wa utoaji wa leseni na vibali vya njia.

174. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barabara ya Kiboje Muembeshauri kwenda Uzini Kituo cha Afya ni miongoni mwa barabara kongwe ambayo ilipata bahati ya kuahidiwa kujengwa na takribani viongozi wa awamu tatu za Serikali yetu, tokea Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

## Wizara ya Afya:

116. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Wilaya ya Micheweni kuimarishwa na kwa sasa inatoa huduma mbalimbali. Hata hivyo, nyumba za madaktari zilizokuwepo zamani katika hospitali hiyo zimevunjwa bila ya kujengwa nyengine badala yake.

Je, ni lini nyumba za madaktari zitajengwa nyengine katika hospitali hiyo, ili madaktari hao waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

142. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ilipoamua kuijenga Hospitali ya Jadida Wete, iliomba eneo na kufungua kituo cha muda katika mtaa wa Ayeya hapo Jadida, ili kuendelea kutoa huduma za matibabu kwa wananchi wake. Hata hivyo, kituo hicho kipo katika makaazi ya watu, huku mabendeji ya vidonda na taka nyengine za wagonjwa zikitupwa katika jaa maarufu la Jadida Msingini.

(a) Je, Serikali ilichukua mazingatio gani kabla ya kukifungua kituo hicho cha muda.

(b) Serikali inatoa kauli gani juu ya usalama wa wananchi kutokana na taka zinazotupwa katika jaa la Jadida Msingini.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

129. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Sheria ya Maji, Namba 5 ya mwaka 2006, kifungu cha 3(1), kifungu cha 4 na kifungu cha 5 vinaainisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, kazi na majukumu ya ZAWA yamehamishiwa kwa Kampuni ya Rand Water.

(a) Je, ni ipi hadhi na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa sasa.

(b) Je, ni ipi tathmini ya ufanisi na kiutawala wa kuhamisha majukumu ya ZAWA kwa Kampuni ya *Rand Water*.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

194. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Mwakilishi Jimbo la Ole) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kama tunavyojua kwamba Bustani ya Forodhani ni kivutio kikubwa na sehemu ya wageni hata wazawa kupumzika na kupata chakula muda wa jioni.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kero na changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na

wajasiriamali wa Forodhani.

(b) Je, Serikali ina mpango upi wa kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo wadogo wazawa waliopo katika Bustani ya Forodhani, ili waone tija na faida ya biashara zao wanazozifanya.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

169. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kutokana na maendeleo makubwa katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Serikali imeendelea kuanzisha na kutekeleza mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha, kuharakisha na kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi.

(a) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani mahasusi wa kuhakikisha uendelevu (sustainability) wa mifumo ya TEHAMA inayoanzishwa.

(b) Katika mifumo ya kidijitali iliyoanzishwa na Serikali, ni mifumo gani kwa sasa umetengezewa Kitabu cha Mtumiaji (User Manual) na Kitabu cha Kitaalamu (Technical Manual).

## II. <u>HOJA ZA SERIKALI</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>**

Mjadala wa Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2025 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**Zanzibar,**
**13 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>**